

# HADITHI YA IBRAHIMU (SEHEMU YA 4 KATI YA 7): KUHAMA KWAKE KWENDA KANAANI

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Mabishano ya Ibrahimu na mfalme, na amri ya Mungu kuhamia Kanaani.

**Aina:** [Makala Imani za Uislamu](#) [Hadithi za Mitume](#)

**Na:** Imam Mufti

**Iliyochapishwa mnamo:** 10 Dec 2021

**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 28 Jan 2022

Uvumbuzi wa kisasa wa kiakiolojia unaonyesha kuhani mkuu alikuwa binti wa mfalme. Kwa kawaida, angefanya jambo la kufanya kielelezo kwa mwanaume aliyelitia unajisi hekalu lake. Muda sio mrefu Ibrahimu, angali kijana<sup>[1]</sup>, alijikuta akihukumiwa, akiwa amesimama peke yake mbele ya mfalme, labda Mfalme Nimrodi. Hata baba yake hakuwa upande wake. Lakini Mungu alikuwa, kama alivyokuwa siku zote.

## Mabishano na Mfalme

Ingawa wana mapokeo wa Kiyahudi-Kikristo wanadai kwa uwazi kwamba Ibrahimu alihukumiwa kuchomwa moto na mfalme, Nimrodi, Quran haifafanui jambo hili. Hata hivyo inataja mabishano ambayo mfalme mmoja alikuwa nayo na Ibrahimu, na baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu wanapendekeza kwamba alikuwa Nimrodi huyu huyu, lakini ni baada ya jaribio lililofanywa na umati la kumuua Ibrahimu<sup>[2]</sup>. Baada ya Mungu kumwoko Ibrahimu kutoka kwa moto, kesi yake iliwasilishwa kwa mfalme, ambaye kwa ujinga wake, alishindana na Mungu mwenyewe kutokana na ufalme wake. Alijadiliana na kijana, kama Mungu anavyotuambia:

***"Hukumwona yule aliye hojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme?" (Quran 2:258)***

Mantiki ya Ibrahimu haikuwa na shaka,

***"Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na kufisha." Yeye akasema: 'Mimi pia nahuisha na kufisha.'" (Quran 2:258)***

Mfalme akaleta watu wawili waliohukumiwa kifo. Alimwachilia mmoja na kumhukumu mwingine. Jibu hili la mfalme lilikuwa nje ya muktadha na ni la kijinga kabisa, kwa hiyo Ibrahimu akatoa jingine, ambalo bila shaka lingemnyamazisha.

***"Ibrahim akasema: 'Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi.' Akafedheheka yule aliye kufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu." (Quran 2:258)***

## **Ibrahimu katika Kuhama**

Baada ya miaka ya wito usiokoma, kukabiliwa na kukataliwa na watu wake, Mungu alimwamuru Ibrahimu kujitenga na familia yake na watu wake.

***Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao: "Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake." (Quran 60:4)***

Angalau watu wawili katika familia yake walikubali, hata hivyo, walikubali mawaidha yake - Lutu, mpwa wake, na Sara, mke wake. Hivyo, Ibrahimu alihama pamoja na waumini wengine.

***"Lut'i akamuamini, na akasema: 'Mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.'" (Quran 29:26)***

Waliamia pamoja kwenye nchi iliyo barikiwa, nchi ya Kanaani, au Shamu Kubwa Zaidi ambako, kulingana na mila za Kiyahudi-Kikristo, Ibrahimu na Loti waliwagawanya watu wao magharibi na mashariki mwa nchi waliyokuwa wamehamia.[\[3\]](#)

***"Na tukamwokoia yeye na Luut'i tukawapeleka kwenye nchi tulio ibariki kwa ajili ya walimwengu wote." (Quran 21:71)***

Ilikuwa hapa, katika nchi hii iliyobarikiwa, ambapo Mungu alichagua kumbariki Ibrahimu kwa uzao.

***"...Naye tukampa Is-haq, na Yaaqub kuwa ni ziada. Na wote tukawajaalia wawe watu wema." (Quran 21:72)***

***"Na hizo ndizo hoja zetu tulizo mpa Ibrahim kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo tumtakaye. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye hikima na Mwenye ujuzi. Na tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wafanyao wema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema. Na Ismail, na Al Yasaa, na Yunus, na Lut'. Na wote tuliwafadhilisha juu ya walimwengu wote. Na kutokana na baba zao, na vizazi vyao na ndugu zao. Na tukawateuwa na tukawaongoa kwenye Njia iliyo nyooka. Hiyo ni hidaya ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo humhidi***

**amtakaye katika waja wake. Na lau wangeli mshirikisha yangeli waharibikia waliyo kuwa wakiyatenda. Hao ndio tulio wapa Vitabu na hukumu na Unabii...." (Quran 6:83-89)**

Manabii waliochaguliwa kwa ajili ya mwongozo wa nchi yake:

**"Na tukawafanya maimamu wakiongoa watu kwa amri yetu. Na tukawafunulia watende kheri, na washike Swala, na watoe Zaka; na walikuwa wanatuabudu Sisi tu." (Quran 21:73)**

---

Rejeleo la maelezo:

[1] Mapokeo ya Kiyahudi-Kikristo yanamwambia kuwa ana umri wa miaka hamsini. *Maandiko: Uteuzi*, H. Polano. (<http://www.sacred-texts.com/jud/pol/index.htm>)

[2] *Hadithi za Mitume*. Ibn Katheer. Machapisho ya Darussalam.

[3] Kitabu cha Kiyahudi: Ibrahimu

Anwani ya wavuti ya makala hii:

<https://www.islamreligion.com/sw/articles/294/hadithi-ya-ibrahimu-sehemu-ya-4-kati-ya-7>

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2023 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.